# JARIDA la Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo la 11 | Januari - Machi 2025



## MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA: SERIKALI MTANDAO YAZIDI KUIMARIKA

- Tanzania yang'ara Duniani utoaji wa huduma za Serikali kidijitali
- Miundombinu shirikishi ya TEHAMA yazidi kuimarika

ega_tanzania | ega online tv

# Yaliyomo

Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu........iii
Miaka Minne ya Rais Dkt. Samia: Serikali Mtandao yazidi kuimarika........1
Dkt. Mpango azitaka Taasisi za Umma Kujiunga na GovESB........4
Taasisi vinara utekelezaji wa Serikali Mtandao zapewa Tuzo........5
Obed Makombe: Mfanyakazi bora e-GA 2024/2025........7
Ongezeni kasi ya Matumizi ya TEHAMA : Simbachawene........8
Wasemavyo wadau wa Serikali Mtandao........9
Maazimio ya Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao........10
e-GA yatoa vifaa tiba kwa Wajawazito........11
Imarisheni Uadilifu kazini : Mhandisi Ndomba........12
TEHAMA inachochea mabadiliko ya kweli kwa vijana : Frank Alex........13
Watumishi waaswa kulinda Afya zao........15
Matukio katika picha ........16




## Kutoka Kwa Mkurugenzi Mkuu

Karibu katika toleo la kumi na moja la Jarida la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika toleo hili la 11 utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi husika, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za Serikali Mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini, inayosaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini na utoaji wa huduma bora kwa umma.

Hali kadhalika, katika Jarida hili utafahamu juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.


Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu jitihada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza.

Nakutakia usomaji mwema.

Mhandisi Benedict B. Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

# MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA: SERIKALI MTANDAO YAZIDI KUIMARIKA




***Na Catherine Peter***

Ilikua Machi 19 Mwaka 2021, siku ambayo historia iliandikwa baada ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuapishwa na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kisha kuanza rasmi safari ya kuiongoza Serikali ya Awamu ya Sita.

Hatimaye imetimia Miaka minne (4) sasa, tangu Mhe. Dkt. Samia alipoanza safari ya kuliongoza taifa letu pendwa la Tanzania, alianza kwa kuweka vipaumbele mbalimbali vya kitaifa ili kuwa na maendeleo endelevu, huku akisisitiza uzalendo, umoja, mshikamano na kuweka wazi nia yake ya kuijenga Tanzania ya kidijitali.

Katika kuhakikisha dhamira ya ujenzi wa Serikali ya Kidijiti inatimia, moja ya vipaumbele alivyoviweka ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini, kwa kuhakikisha TEHAMA inatumika vyema kwenye utendaji kazi, ili kuongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Benedict Ndomba, amebainisha kwamba kumekuwa na mafanikio chanya katika matumizi ya TEHAMA Serikalini, ambayo yamechochewa na utayari wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Mhandisi Ndomba amebainisha kuwa, uwepo wa dira mahususi kuhusu Matumizi ya TEHAMA, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, pamoja na mikakati madhubuti inayosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kumechochea kuimarika zaidi kwa matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma.

Mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kutambuliwa kimataifa katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini ambapo, Mwaka 2022, **Benki ya Dunia (WB)** ilifanya utafiti katika nchi 198 Duniani ikiwemo Tanzania, kuhusu Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani, katika Utoaji wa Huduma za Serikali na Ushirikishwaji wa Wananchi **(GovTech Maturity Index).**

Ripoti ya utafiti huo ilibainisha kuwa, Tanzania imefanikiwa kupanda daraja kutoka kundi B hadi kundi A na kushika nafasi ya 26 Duniani, nafasi ya pili (2) barani Afrika baada ya Mauritius na ya kwanza katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Aidha, ripoti hiyo ilionesha kuwa, mafanikio haya yalitokana na utayari wa Serikali wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, uwepo wa dira mahusus kuhusu matumizi ya TEHAMA, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, Mikakati madhubuti na utekelezaji wake unaosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Vilevile, mwaka 2024 Tanzania ilishinda tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 'UN Public Service Innovation Awards' kupitia Mfumo wa e-Mrejesho, ambao ulitambuliwa na umoja huo kama jukwaa shirikishi la kidijitali linalowezesha Serikali, kukusanya maoni ya wananchi na hivyo kuweza kuifanya Serikali kuwa karibu zaidi na wananchi wake na kuwapa huduma bora.

Mafanikio mengine yaliyopatikana chini ya uongozi wa Dkt. Samia, ni ujenzi wa Miundombinu na rasilimali shirikishi za TEHAMA ikiwemo Mkongo wa Taifa (NICTBB), Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GovNet), Vituo vya Kitaifa vya Data na Masafa ya Intaneti, inayoziwezesha Taasisi za Umma kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA.

Mhandisi Ndomba anafafanua




kuwa, matumizi ya Mifumo na Miundombinu shirikishi yamesaidia kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma pamoja na kuhakikisha uwepo wa usalama wa mawasiliano Serikalini.

“Kutokana na uongozi bora wa Awamu ya Sita, Mamlaka imefanikiwa kujenga, kuboresha na kusimamia uendeshaji wa Vituo vya Serikali vya Kuhifadhi Mifumo na Taarifa (Government Data Center), ambapo hadi sasa vituo hivyo vinatumiwa na taasisi za umma kuhifadhi Mifumo na taarifa zao kwa usalama wa uhakika,” alifafanua Mhandisi Ndomba.

Katika kuhakikisha anaijenga Tanzania ya Kidijitali, Mhe. Rais ameelekeza Mifumo ya TEHAMA kuwasiliana na kubadilishana taarifa, ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi sambamba na kupunguza mianya ya rushwa, kuondoa urasimu, na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Serikali.

e-GA imetekeleza agizo la Mhe. Rais, kwa kujenga na kusanifu Mfumo wa pamoja wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus – GoVESB), ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inawasiliana na kubadilishana taarifa.

Pamoja na utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais, ujenzi wa mfumo wa GovESB pia ni utekelezaji wa Kifungu na. 48 cha Sheria ya Serikali Mtandao Namba. 10 ya Mwaka 2019, ambayo inaielekeza Mamlaka kutengeneza Mfumo shirikishi, utakaowezesha Mifumo ya Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Hadi sasa, taasisi mbalimbali za umma zimeunganishwa na Mifumo ya taasisi hizo inawasiliana na kubadilishana taarifa. Ubadilishanaji wa taarifa kupitia Mfumo huu, umechochea kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma, na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mhandisi Ndomba ameongeza kuwa, kwa upande wa kisekta, Mfumo wa GovESB umeleta matokeo chanya katika Sekta ya Hakijinai ambapo, baadhi ya taasisi za Hakijinai zinawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia mfumo wa GovESB, kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (NPS), MAHAKAMA na Jeshi la Polisi.

‘’Vilevile, Mfumo wa Taifa wa Ununuzi Kielektroniki (NeST) umeunganishwa na Mifumo ya Taasisi 17 zikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Leseni na Biashara (BRELA) na Benki Kuu ya Tanzania

(BoT), ili kuwezesha usimamizi wa ununuzi wa umma kwa ufanisi na urahisi zaidi,"amefafanua Mhandisi Ndomba.

Pia, Mamlaka imeshirikiana na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) katika kuunganisha sekta ya elimu, ambapo mfumo wa tume hiyo, umeunganishwa na Mifumo ya Taasisi za Elimu 94 ambapo, taasisi 64 ni za umma na taasisi 30 ni za binafsi, ili kuwezesha na kurahisisha mchakato wa udahili na mahitaji mengine kwenye sekta ya elimu.

"Kwa upande wa sekta ya afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeunganishwa na taasisi mbalimbali zinazohusika na utoaji wa huduma za afya zikiwemo hospitali", amebainisha Mhandisi Ndomba.

Aidha, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imeunganishwa na Mifumo ya watoa huduma wengine wa sekta za umma na binafsi zikiwemo Benki kwa ajili ya utambuzi wa wateja, ili kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi zaidi.

"Pamoja na hayo, tumetengeneza Mifumo shirikishi inayotumiwa na taasisi mbalimbali za umma ukiwemo Mfumo Jumuishi wa Utoaji wa Huduma za Serikali kwa njia ya Simu za Mkononi (m-GOV) unaorahisisha, na kuharakisha utoaji wa huduma kwa wananchi." Amefafanua Mhandisi Ndomba.

Mfumo huu wa m-GOV umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mkononi nchini na unatoa huduma za ujumbe mfupi wa maandishi (SMS), kwa kutoa na kupokea taarifa kupitia namba jumuishi ambayo ni **15200 na 15201,** pamoja na huduma za menyu ya namba ya msimbo (USSD) kupitia namba jumuishi ***152*00#".**

Mhandisi Ndomba ameainisha Mifumo mingine iliyotengenezwa na e-GA ikiwemo Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-office), ambao unarahisisha shughuli za mzunguko wa mafaili na nyaraka ndani ya Taasisi za Umma, na Mfumo wa e-Board unaowezesha uratibu wa shughuli zote za uandaaji wa vikao vya bodi na menejimenti katika Halmashauri na Taasisi za Umma.

Tumetengeneza Mfumo wa e-Mikutano unaowezesha watumishi wa umma kufanya vikao kidijitali mahali popote, bila kulazimika kukutana mahali pamoja, na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uandaaji na uendeshaji wa vikao.

Pia tumetengeneza Mfumo wa e-Dodoso, unaomuwezesha mwananchi au taasisi kutengeneza na kujaza dodoso, kupata tathmini pamoja na takwimu za dodoso kwa njia ya mtandao," ameongeza Mhandisi Ndomba.

Sanjari na hilo, ujenzi na uendeshaji wa Mifumo na Miundombinu hii, hufanywa kwa kutumia wataalamu wazawa, na hivyo kusaidia kuokoa fedha nyingi za kigeni za Serikali ambazo zilitumika kununua Mifumo kutoka kwa wakandarasi wa nje ya nchi kwa gharama kubwa.

Aidha, usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA ni jambo muhimu linalozingatiwa na Mamlaka katika ulimwengu huu wa Kidijitali ambapo, kumekuwa na mashambulizi mengi ya kimtandao.



**"Katika kukabiliana na matishio ya usalama wa mitandao, Mamlaka hutoa msaada wa kiufundi kuhusu usalama wa TEHAMA kwa taasisi za umma, ushauri kuhusu viashiria (alerts) mbalimbali za matishio mapya ya usalama mtandao (emerging cybersecurity threats) kwa taasisi za umma".**

Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Mhandisi Ndomba ameongeza kuwa e-GA pia inawajibika kufanya utatuzi wa mashambulio ya kimtandao pindi yanapotokea (ICT security incidents response) pamoja na kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA Serikalini kuhusu usalama wa mtandao.

Aidha, ili kuhakikisha Mifumo na Miradi ya TEHAMA Serikalini inaleta tija iliyokusudiwa, Mamlaka huandaa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ambayo taasisi za umma zinatakiwa kuifuata wakati wote wa uandaaji na uendeshaji wa miradi hiyo.

Sambamba na hilo, e-GA imeimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), katika utekelezaji wa jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao.

Aidha, Mhandisi Ndomba ameahidi kuimarisha na kuendeleza ushirikiano wa pande hizo mbili, ili kuhakikisha ukuaji wa Serikali Mtandao unazidi kuimarika bara na visiwani.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa eGAZ Bw. Said Seif Said, amesema ushirikiano uliopo kati ya e-GA na eGAZ umekuwa chachu ya mageuzi ya Kidijitali ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ikiwa ni pamoja na uwepo wa Mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo inatumika pia Zanzibar.

"Tangu tuliposaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na e-GA tumepiga hatua kubwa sana, mabadiliko yamepatikana na yanaonekana," amesema Bw. Said.

Hata hivyo, Bw. Said amempongeza Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi Ndomba, kwa uongozi mahiri na timu nzima ya e-GA kwa ushirikiano kuhakikisha Zanzibar inanufaika na maendeleo ya Kidijiti.

Bw. Said ametaja baadhi ya Mifumo inayotumika Zanzibar ambayo ni sehemu ya mashirikiano hayo ni pamoja na, Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS) na Mfumo wa vibali vya Watumishi wa Umma kusafiri nje ya nchi (e-Vibali).

Mifumo mingine ni ule wa ukusanyaji mapato (ZanMalipo), Mfumo wa kutoa Ankara za Maji (MAJIIS), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Kusimamia Utendaji Kazi na Rasilimali za Taasisi (ERMS) na Mfumo wa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi (e-Wawakilishi).

Mafanikio haya ya Serikali Mtandao, yanatokana na usimamizi mzuri, utayari na uwekezaji unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kuhakikisha Serikali Mtandao inazidi kuimarika zaidi na kuleta tija iliyokusudiwa.




# DKT. MPANGO AZITAKA TAASISI ZA UMMA KUJIUNGA NA GOVESB

*Na Queenter Mawinda*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Philip Mpango, amezielekeza Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali, ili kurahisisha utendaji kazi katika taasisi zao na utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi kwa urahisi na gharama nafuu zaidi.

Dkt. Mpango alisema hayo Februari 11 mwaka huu, wakati akifungua Kikao Kazi cha 5 cha Serikali Mtandao, kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Takribani wadau 1,500 walishiriki kikao hicho wakiwemo Maafisa Masuuli, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya TEHAMA, Maafisa TEHAMA na watumiaji wengine wa mifumo ya TEHAMA kutoka katika Taasisi, Halmashauri na Mashirika mbalimbali ya Umma.

Dkt. Mpango alisisitiza kuwa, ili kuleta mapinduzi ya kidijitali Serikalini na matumizi endelevu ya TEHAMA, Taasisi za Umma zinapaswa kujiunga na Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus - GoVESB).

Aidha, Dkt. Mpango alizitaka Taasisi za Umma, ambazo hazijahuisha taratibu za utendaji kazi wake (Business processes), kuhakikisha zinafanya hivyo ili, kuweza kujenga Mifumo inayowasiliana na kubadilishana taarifa kwa urahisi.

"Ili Taasisi za Umma ziweze kuwasiliana na kubadilishana taarifa, ni lazima taratibu za utendaji kazi wa taasisi ziandaliwe na kuwekwa kwenye maandishi, hivyo ni lazima kuhakikisha kila taasisi inatekeleza agizo hili," alisisitiza Dkt. Mpango.

Alibainisha kuwa, katika kuhakikisha mifumo ya afya inawasiliana na kubadilishana taarifa, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), tayari imendaa taratibu za utendaji zilizoboreshwa, ikiwa ni kuelekea hatua ya kuwa na Mfumo utakaoweza kutumiwa na Hospitali nyingi kwa pamoja.

**"Tunategemea kuona mgonjwa anayetibiwa Hospitali ya Mount Meru hapa Arusha anapokwenda Muhimbili, Daktari aweze kuona taarifa za historia ya mgonjwa moja kwa moja kutoka Hospitali ya Mount Meru kupitia Mfumo,"**

Dkt. Philip Mpango
**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Aidha, Dkt. Mpango alizitaka sekta nyingine kuiga mfano wa Wizara ya Afya, kwa kuhuisha taratibu zake ili kuchochea mageuzi ya kidijitali katika utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwa haraka na gharama nafuu.

Vilevile, Dkt. Mpango alipongeza e-GA kwa kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluh Hassan, kwa kusanifu na kujenga Mfumo wa GoVESB, ambao umeleta matokeo chanya katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Haki Jinai.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene, alisema kuwa, Serikali imewekeza katika TEHAMA, kwakuwa ni nyenzo muhimu katika kuleta utawala bora na kuongeza ufanisi Serikalini, ili kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Waziri alisema, matumizi ya TEHAMA Serikalini yamesaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za Serikali hivyo kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi kwa wakati.

Kikao Kazi cha Tano cha Serikali Mtandao kiliongozwa na kauli mbiu isemayo, **"Jitihada na ubunifu wa Serikali Mtandao kwa utoaji huduma za umma kwa ufanisi"** ili kuchochea matumizi ya bunifu mbalimbali za TEHAMA, itakayosaidia utoaji wa huduma za umma kwa ufanisi.

# TAASISI VINARA UTEKELEZAJI WA SERIKALI MTANDAO ZAPEWA TUZO




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango (kulia), akimkabidhi tuzo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Kuwe Bakari (kushoto), baada ya kuibuka mshindi wa Taasisi Hodari kwenye Matumizi ya TEHAMA katika kuwashirikisha Wananchi.

*Na Queenter Mawinda*

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetoa tuzo mbalimbali kwa Taasisi za Umma zilizofanya vizuri katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kuchochea matumizi ya TEHAMA Serikalini.

Tuzo hizo zilitolewa Februari 13 mwaka huu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb), wakati akifunga Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao, kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) jijini Arusha.

Aidha, tuzo hizo ziligawanywa katika makundi matatu ya utekelezaji wa Serikali Mtandao ambapo kundi la kwanza lilikuwa ni Uzingatiwaji wa Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao **(Best Performance in Compliance to e-Government Act, Standards and Guidelines).**

Kundi hili liliangalia maeneo mawili ambayo ni Taasisi zilizopo katika ngazi ya NNE ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini (Level 4 of e-Government Capability Maturity) na Taasisi zilizopo katika ngazi ya TATU ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini (Level 3 of e-Government Capability Maturity Framework)

Katika ngazi ya NNE ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini, taasisi nne ziliibuka na ushindi ambazo ni Wizara ya Katiba na Sheria ikishika nafasi ya kwanza, ikifuatiwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) mshindi wa pili, Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) mshindi wa tatu na Mamlaka ya Bandari (TPA) mshindi wa nne.

Aidha, kwa upande wa Taasisi zilizo katika ngazi ya TATU ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini, Halmashauri ya Wilaya ya Geita iliibuka mshindi wa pekee.

Kundi la pili ni Taasisi Hodari kwenye Matumizi ya TEHAMA katika kuwashirikisha Wananchi (Best Performance in Utilization of ICT for Citizen Engagement), washindi wa kundi hili walikuwa ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambayo iliibuka kinara kwa kushika nafasi ya kwanza, huku nafasi ya pili ikishikwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ikishika nafasi ya tatu.

Kundi la tatu lilihusu Taasisi Kinara katika Kuunganisha na Kubadilishana Taarifa, kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Servise Bus – GoVESB) ambapo Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) liliibuka na ushindi wa pekee.

Washindi wa tuzo hizo wameipongeza e-GA kwa uandaaji wa tuzo hizo, kwa kuwa zinatoa hamasa na ushindani chanya wa matumizi ya TEHAMA Serikalini, hali ambayo inasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

**“Tunaishukuru e-GA kwa kuandaa tuzo hizi kwani zitasaidia kuchochea uzingatiaji wa Sheria ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma”.**

Bw. Abdulatif Minhajj
**Mkurugenzi wa TEHAMA - TPA**

Bw. Minhajj ameongeza kuwa tuzo hizo zitaimarisha jitihada zilizopo za



Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao wa e-GA Bi. Sultana Seiff, akieleza namna zoezi la tuzo lilivyoendeshwa

Bandari katika kufuata Miongozo mbalimbali ya Serikali Mtandao, katika uendeshaji na usimamizi wa mifumo ya TEHAMA bandarini.

Aidha, Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao wa e-GA Bi. Sultana Seiff, alibainisha vigezo mbalimbali vilivyotumika katika ushindani katika kundi la kwanza kuwa ni maeneo mawili ambayo ni Taasisi zilizopo katika ngazi ya NNE ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini, na Taasisi zilizopo katika ngazi ya TATU ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini.

Bi. Sultana alisema kuwa katika kundi la pili la Taasisi Hodari kwenye Matumizi ya TEHAMA katika kuwashirikisha Wananchi, vigezo vilivyoangaliwa ni pamoja na Taasisi zilizounganishwa na Mfumo wa Kutuma, Kupokea na Kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi (e-Mrejesho), Idadi ya malalamiko yaliyopokelewa na Taasisi zinazotumia mfumo huo, alama za ushughulikiaji wa malalamiko inayohusisha idadi ya malalamiko yaliyofungwa na idadi ya malalamiko yanayoendelea kushughulikiwa.

Vilevile Bi. Sultana alisema katika kundi la tatu, Mamlaka iliangalia Taasisi zinazobadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB), tarehe ya kujiunga na mfumo huo, idadi ya maombi ya maunganisho yaliyopokelewa na Taasisi husika, muda unaotumika kuidhinisha maombi ya maunganisho kutoka Taasisi mbalimbali na asilimia ya miamala ya ubadilishanaji taarifa iliyofanyika kikamilifu.

Bi. Sultana ametoa rai kwa Taasisi zote za Umma kuongeza jitihada katika uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kuwezesha matumizi sahihi ya TEHAMA katika taasisi zao yatakayoleta tija katika utendaji kazi.

**"Ni matumaini yangu kuwa Taasisi za umma zitaiga mfano wa Taasisi zilizofanya vizuri katika maeneo mbalimbali, yaliyoshindanishwa na mwakani tunatarajia idadi ya Tuzo zitaongezeka".**

Bi. Sultana Seiff
**Meneja wa Usimamizi wa Udhibiti na Viwango vya Serikali Mtandao**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Goerge Simbachawene (kushoto), akimkabidhi tuzo Mkurugenzi wa TEHAMA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Abdulatif Minhajj (kulia) baada ya kuibuka mshindi wa tatu katika ngazi ya NNE ya Ukomavu wa TEHAMA Serikalini.



# OBED MAKOMBE: MFANYAKAZI BORA e-GA 2024/2025

*Na Queenter Mawinda*

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imemtangaza Afisa TEHAMA Bw. Obed Makombe kuwa mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 huku uwajibikaji na weledi vikitajwa kuwa msingi mkuu wa ushindi huo.

Uchaguzi wa mfanyakazi bora wa Mamlaka ulifanyika Februari 26, mwaka huu, baada ya kuwashindanisha wafanyakazi bora 10 kutoka katika idara na vitengo, na kisha Menejimenti kupiga kura ili kumpata mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi. Benedict Ndomba amesema, zoezi la uchaguzi wa mfanyakazi bora hulenga kuchochea utendaji kazi wenye kuzingatia uadilifu na weledi kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mhandisi. Ndomba alisema kuwa, e-GA inatambua na kuthamini mchango wa watumishi wake wote katika kufikia malengo ya taasisi na kuwa, uchaguzi wa mfanyakazi bora ni motisha kwa wafanyakazi wote kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi na weledi huku wakizingatia misingi mikuu ya Mamlaka.



**"Mamlaka inatambua na kuthamini mchango wa watumishi wote katika kufanikisha malengo ya Taasisi, hivyo nitoe rai kwa watumishi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu lakini pia niwapongeze sana watumishi bora waliochanguliwa kwa mwaka huu wa 2024/2025".**

Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Alibainisha kuwa, Mamlaka itaendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya kazi ikiwemo, kutoa vitendea kazi kwa wakati, chakula na mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wake ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Naye, Meneja Rasilimaliwatu na Utawala Bw. Erick Kalembo alisema, Mamlaka ilifanya uchaguzi wa ndani kwa kila Idara na vitengo ili kupata mfanyakazi bora na kisha orodha hiyo iliwasilishwa Menejimenti kwa ajili ya kumchagua mfanyakazi bora wa taasisi.

Alisema, Menejimenti iliwapima watumishi wote bora waliochaguliwa kutoka kwenye Idara na Vitengo na kisha kupiga kura kwa uwazi ili kumchagua mfanyakazi bora wa Mamlaka, kwa kuzingatia vigezo vilivyopo bila upendeleo wa aina yeyote.

Uchaguzi huo ulifanyika kwa kupiga kura na kuwapata washindi watatu walioingia tatu bora na hatimaye kumpata mfanyakazi bora wa jumla wa Taasisi.

"Tuliangalia vigezo mbalimbali vya mfanyakazi bora ikiwemo nidhamu, uadilifu na utekelezaji wa majukumu ya mtumishi kupitia mfumwa upimaji kwa watumishi wa e-SS", alisema Bw. Kalembo.

Naye Mfanyakazi bora wa Mamlaka Bw. Obed Makombe, ametoa shukrani zake kwa watumishi na menejimenti ya Mamlaka kwa kutambua juhudi na utendaji kazi wake, uliopelekea kuchagulia kupata ushindi huo.

Nafasi ya pili imeshikwa na **Bw. Melkizedeck Ndabayoye**(Afisa Tawala Mwandamizi) kutoka Idara ya Huduma za Uwezeshaji na nafasi ya tatu kushikwa na **Bw. Kulwa Gibaka** (Mhasibu) kutoka Idara ya Uhasibu na Fedha.

**"Napenda kuwashukuru watumishi wenzangu kwa kutambua utendaji kazi wangu lakini pia nawashukuru kwa ushirikiano wao kwani katika taasisi hata ukiwa mfanyakazi bora ni lazima ushirikiane na wafanyakazi wengine ili kufikia malengo ya taasisi, naahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi zaidi"**

Obed Cassian Makombe
**Afisa TEHAMA**

# ONGEZENI KASI YA MATUMIZI YA TEHAMA: SIMBACHAWENE




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Goerge Simbachawene (Mb), akitoa hotuba wakati wa kufunga Kikao Kazi cha 5 cha Serikali Mtandao.

***Na Queenter Mawinda***

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb), amezitaka Taasisi za Umma zenye kiwango kidogo cha utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao, kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA ili kuleta tija katika utendaji kazi wao.

Mhe.Simbachawene ametoa kauli hiyo Februari 13 mwaka huu, wakati akifunga Kikao Kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa muda wa siku tatu katika ukumbi wa AICC jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki takriban **1500** kutoka katika taasisi za umma na binafsi. Alisema kuwa, Serikali imedhamiria kuimarisha na kupanua wigo wa matumizi TEHAMA, ili kwenda sambamba na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwa kuwa shughuli nyingi duniani zikiwemo za kiuchumi kwa sasa zinafanyika kwa kutumia TEHAMA.

Waziri Simbachawene alibainisha kwamba, Serikali imeweka kipaumbele kwenye matumizi ya TEHAMA hususan katika masuala ya utafiti na ubunifu, ili kuwa na mifumo ya TEHAMA itakayotatua changamoto zilizopo nchini kwa ufanisi zaidi kulingana na mazingira husika.

"Pamoja na hayo tumedhamiria kuimarisha usalama wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini pamoja na kuongeza idadi ya watumiaji wa intaneti, ili kuhakikisha wananchi wanazifikia huduma za Serikali kidijitali mahali walipo," alisema Simbachawene.

Aliongeza kuwa, kutokana na kasi ya ongezeko la matumizi ya simu za mkononi, Wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imejipanga kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma nyingi za serikali, zinapatikana kupitia simu za mkononi.

**"Tunajivunia kuona idadi ya watumiaji wa simu za mkononi pamoja na intaneti inaongezeka mwaka hadi mwaka, ongezeko hili linatupa chachu ya kuboresha upatikanaji wa huduma za Serikali kupitia simu za mkononi ili ziwafikie wananchi wengi zaidi na kwa urahisi."**

Mhe. George Simbachawene (Mb)
**Waziri - UTUMISHI**

Aidha, Mhe. Simbachawene alizielekeza taasisi za umma kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha zinatumia fursa ya ongezeko hili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kidijitali kupitia simu za mkononi.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu Bw. Mulula Mahendeka alisema, vikao kazi vya Serikali Mtandao vinavyofanyika kila mwaka, vimekuwa na manufaa makubwa katika kukuza na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao, kupitia mawazo mbalimbali yanayotolewa na washiriki wa vikao hivyo.


Alibainisha kuwa, katika kila kikao kumekuwa na maazimio yanayowekwa na washiriki yanayolenga kuboresha ukuaji wa Serikali Mtandao nchini, na kuahidi kusimamia utekelezaji wa maazimio ya Kikao Kazi cha 5 cha Serikali Mtandao.

**"Niwaahidi washiriki wote kuwa Wizara itasimamia utekelezaji wa maazimio yote mliyoyaweka katika katika Kikao Kazi hiki ikiwa maazimio hayo yanaihusu Wizara yenyewe, e-GA au taasisi nyingine ya umma".**

Bw. Mulula Mahendeka
**Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu**

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mhandisi. Benedict Ndomba, aliwashukuru washiriki wa kikao hicho na kuwakumbusha kuzingatia Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika uanzishwaji na uendeshaji wa miradi mbalimbali ya TEHAMA.

# WASEMAVYO WADAU WA SERIKALI MTANDAO



Mifumo ya TEHAMA imesaidia kupunguza gharama katika utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi.

**Zena Athumani**

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano-Bodi ya Michezo ya kubahatisha Tanzania



Upatikanaji wa huduma mbalimbali za Serikali pamoja na ulipaji wa bili za Serikali umerahisishwa kupitia ***152*00#.** Huduma za Serikali kwa sasa zinapatikana kiganjani mwako.

**Bw. Desmond Mayo**

Meneja wa kitengo cha TEHAMA - RUWASA



Serikali ya awamu ya sita (6) imefanikiwa kuwekeza katika TEHAMA na kuwa nyenzo muhimu katika kuleta utawala bora na kuongeza ufanisi Serikalini.

**Dkt. Angelina Miso**

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Mifumo na Huduma za TEHAMA-Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari




Mafuzo mbalimbali yanayotolewa na e-GA yamesaidia kuleta uelewa kwa watumishi wa Serikali kuhusu serikali mtandao, teknolojia mpya zinazoibukia na zinavyoweza kutumika katika kuimarisha utendaji na kurahisisha utoaji wa huduma bora kwa Umma.

**Bw. Emmanuel Tumaini Kidebwala**

Meneja wa TEHAMA-Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

# MAAZIMIO YA KIKAO KAZI CHA TANO (5) CHA SERIKALI MTANDAO



Kikao kazi cha Tano (5) cha Serikali Mtandao cha Mwaka 2025 kilihitimishwa kwa kuwa na Maazimio Sita (6) kama ifuatavyo: -

1. Mamlaka ya Serikali Mtandao ihakikishe kuwa inadhibiti usalama wa Mifumo inayotumika Serikalini.
2. Taasisi za Umma zinapaswa kuandaa na kuweka katika maandishi Taratibu za Utendaji Kazi **“Business Process”** ili kurahisisha ujenzi wa mifumo ya TEHAMA na kuwezesha mifumo ya TEHAMA serikalini iweze kuwasiliana na kubadilishana taarifa”.
3. Mamlaka ya Serikali Mtandao ikamilishe nyenzo ya kupima uelewa wa usalama wa kimtandao kwa watumishi wa umma.
4. Taasisi za umma zihakikishe zinatumia nyenzo ya kupima uelewa wa usalama wa mtandao angalau mara moja kwa mwaka kwa watumishi wa umma wanaotumia mifumo ya TEHAMA.
5. Kuimarisha Mtandao wa mawasiliano ya intaneti ili kuongeza upatikanaji wa mtandao wa intaneti.
6. Taasisi za Umma zijengewe uwezo kwa kutumia teknolojia zinazochipukia **(Emerging Technologies)** katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma.

# e-GA YATOA VIFAA TIBA KWA WAJAWAZITO




Watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao e-GA waliopo ofisi za Dodoma, wakikabidhi msaada wa vifaa tiba na mahitaji muhimu katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani 2025.

*Queenter Mawinda na Catherine Peter*

Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2025, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetoa msaada wa vifaa tiba na mahitaji muhimu kwa wajawazito na akina mama waliojifungua, katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma (General) na Hospitali ya Mbagala ya jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Meneja Mawasiliano wa e-GA Bi. Subira Kaswaga alisema, e-GA inatambua umuhimu wa kumuwezesha mwanamke mwenye uhitaji ili kujenga taifa bora.

Bi. Subira aliongeza kwamba, msaada huo ni moja ya njia inayoonesha namna ambavyo Mamlaka hiyo inavyomthamini mwanamke.

Alisema katika kuhakikisha jamii inapata huduma bora za afya, e-GA imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Afya kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayorahisisha utoaji wa huduma za afya kwa jamii wakiwemo wanawake na watoto.

"Tunatambua kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imewekeza katika sekta ya afya kwa kujenga vituo vya afya pamoja na kuboresha miundombinu yake, nasi e-GA tunaunga mkono jitihada za Serikali kwa kutengeneza mifumo ya TEHAMA, inayorahisisha utendaji kati katika sekta ya afya ili kuwawezesha wananchi kupata huduma za afya kwa urahisi zaidi," alisema Bi. Subira.

Aliongeza kuwa, mifumo ya TEHAMA huimarisha haki na usawa katika utoaji wa huduma za Serikali, bila kujali jinsia au hali ya kiuchumi na kutoa nafasi sawa kwa wote katika kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi na kielimu zinazopatikana katika TEHAMA.

Afisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Dodoma, Bi. Tegemea Ngulwa, na Dkt Ally Mussa Mganga Mfawidhi Hospitali ya Mbagala Rangi Tatu, waliishukuru e-GA kwa msaada huo na kuomba kuendeleza ushirikiano katika kuwasaidia wagonjwa wenye uhitaji katika hospitali hizo.

**"Kama isemavyo kauli mbiu ya mwaka huu juu ya haki usawa na uwezeshaji kwa wanawake, e-GA kupitia Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao hutoa nafasi kwa wanafunzi wa TEHAMA wa vyuo vikuu, kushiriki mafunzo kwa vitendo na mafunzo kazini, hii ni namna moja wapo inayoonesha jinsi gani e-GA tunaishi katika kauli hii ya kuimarisha usawa na haki kwa jinsia zote".**

Bi. Subira Kaswaga
**Meneja Mawasiliano - e-GA**




Watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao e-GA waliopo ofisi za Dar Es Salaam, wakikabidhi msaada wa vifaa tiba na mahitaji muhimu katika hospitali ya Mbagala Rangi tatu wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani 2025.

# IMARISHENI UADILIFU KAZINI: MHANDISI NDOMBA



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba akizungumza wakati wa kikao cha Watumishi kilichofanyika Februari 26 mwaka huu katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam.

*Na Subira Kaswaga*

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wametakiwa kuimarisha na kuendeleza uadilifu kazini ili kuhakikisha Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi zaidi.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo Mhandisi Benedict Ndomba Februari 26 mwaka huu, wakati akifungua kikao cha wafanyakazi wa Mamlaka kilichofanyika katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa, ili Mamlaka iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ni lazima watumishi wake wawe na weledi na uadilifu wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

**"Natambua kuwa, mmekuwa mkizingatia weledi na uadilifu katika kazi zenu lakini hiyo haitoshi, ni lazima muhakikishe mnaimarisha zaidi weledi na uadilifu mlionao sasa, ili kwa pamoja tuweze kufikia malengo ya taasisi tuliyojiwekea".**

Mhandisi Benedict Ndomba
**Mkurugenzi Mkuu e-GA**

Aliongeza kuwa, uimara wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosimamiwa na Mamlaka hiyo hutokana na uadilifu wa watumishi na hivyo, hatari huweza kutokea ikiwa watumishi hao watakosa uadilifu.

"Tunafahamu kuwa matishio ya kiusalama mtandaoni hutokea kila mara duniani kote, ni lazima tuendelee kuyadhibiti ili kulinda mifumo na miundombinu ya TEHAMA tunayosimamia, tunaweza kufanikiwa ikiwa sote tutaendelea kuwa waadilifu," alisisitiza Mhandisi Ndomba.

Naye Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa Mamlaka hiyo CPA. Bw. Salum Mussa alisema, Mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wote ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka.

"Mamlaka itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo mbalimbali ili kuimarisha ujuzi na kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea kila siku," alisema CPA. Bw. Salum Mussa.

Aliongeza kuwa, nia ya Mamlaka ni kuhakikisha kila mtumishi anaendeleza ujuzi alionao kwa kupata mafunzo mara kwa mara kutokana na mahitaji yatakayojitokeza na kuwasihi watumishi kutumia vema fursa hiyo kwa maslahi mapana ya taasisi.

Kwa upande wa watumishi wa Mamlaka walioshiriki kikao hicho, waliupongeza uongozi kwa kuandaa kikao ambacho kiliwakutanisha watumishi wote kwa pamoja na kupata elimu kuhusu mambo mbalimbali yakiwemo afya na uwekezaji.

"Kikao hiki kimekuwa na manufaa makubwa kwani, tumejifunza kuhusu afya ya akili, uwekezaji na masuala ya rushwa kutoka kwa wataalamu wa maeneo hayo, lakini pia tumeona mipango ya taasisi katika kutuendeleza watumishi wake," alisema Bw. Jacob Willy, Afisa TEHAMA Mwandamizi wa e-GA.

Naye Bi. Sara Mgale Afisa Ugavi wa Mamlaka alipongeza e-GA kwa kutenga bajeti ya mafunzo kwa watumishi wake kila mwaka, ili kuhakikisha wanaendeleza na kuimarisha ujuzi wao, hali ambayo imechangia kuongezeka kwa weledi hivyo kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi katika Idara na Vitengo.

Kikao cha watumishi wa Mamlaka kilifanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia Februari 26 hadi 28 mwaka huu, ambapo mada mbalimbali zilizohusu afya, uwekezaji, maadili ya utumishi wa umma pamoja na rushwa, ziliwasilishwa na baadaye kikao hicho kilihitimishwa kwa bonanza la michezo lililofanyika katika viwanja vya Gymkhana.

# TEHAMA INACHOCHEA MABADILIKO YA KWELI KWA VIJANA: FRANK ALEX

**"Bunifu hizi pia zitakuwa ni suluhisho la kupunguza utegemezi kwa nchi za nje na kuongeza uwezo wetu katika sekta za viwanda na uzalishaji"**

Bw. Frank Alex
**Afisa TEHAMA**



Bw. Frank Alex

*Na Benchine Bago*

Ari ya vijana katika kuifahamu na kutumia fursa zilizopo katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), imekuwa ni kichocheo katika kuleta mapinduzi ya kiteknolojia nchini.

Hii inatokana na ukweli kuwa, TEHAMA inazidi kukua kila uchwao na kuvutia vijana wengi kutokana na fursa mbalimbali zinazopatikana zikiwemo za kielimu na kiuchumi.

Kutokana na uwepo wa fursa hizo, vijana wengi hupenda kutumia TEHAMA ili waweze kutimiza ndoto zao za kielimu, kiuchumi sambamba na kuleta mabadiliko chanya katika jamii kupitia TEHAMA.

Frank Alex, ni muhitimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika Shahada ya Uhandisi wa Kompyuta 'Bachelor of Science in Computer Engineering' ambaye kwa sasa, anajitolea katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (e-GOVRIDC) cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Alianza kupenda masomo ya TEHAMA, pale alipoamua kujiunga na klabu ya kompyuta alipokuwa shule ya Sekondari ya Benjamin William Mkapa iliyopo jijini Dar-es-Salaam.

Kujiunga kwake katika Klabu hiyo, ndiyo ulikuwa mwanzo wa safari yake ya kutaka kuleta mageuzi ya TEHAMA nchini, na kuwa miongoni mwa kundi la vijana wanaoamini katika matumizi sahihi ya TEHAMA, ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii yakiwemo ya kielimu, afya, kiuchumi n.k.

**"TEHAMA hutumika kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika jamii yetu, na kwa msingi huo sisi vijana tunaamini kuwa tukijiendeleza katika fani hii kwa ufanisi mzuri, tunaweza kuchangia mageuzi ya kitaifa katika sekta mbalimbali zikiwemo afya, elimu, uchumi na nyinginezo."**

Bw. Frank Alex
**Afisa TEHAMA**

Anabainisha kuwa, mapenzi yake katika TEHAMA hayakuja kwa bahati mbaya, bali uwepo wa sababu nyingi zilizomfanya awe na hamu ya kujifunza na kujitosa katika uwanja huu.

Shauku yake kubwa ilikuwa ni kujua jinsi mambo yanavyofanya kazi, jinsi kompyuta na teknolojia nyingine zinavyotengenezwa na kama hiyo haitoshi, ni pale alipowaona vijana wenzake wakipata mafanikio makubwa kupitia TEHAMA na hivyo kumuongezea shauku ya kutaka kujifunza zaidi.

"Niliona vijana walionitangulia wakitengeneza tovuti, programu za simu, au hata kujiunga na fursa za kujiajiri kupitia intaneti (mtandao), na hili lilinifanya niwe na nia ya kutaka kufanikiwa kama wao", anafafanua Bw. Frank.

Mtaalamu huyu chipukizi anasema, mapenzi na TEHAMA yaliongezeka zaidi baada ya kugundua kwamba TEHAMA ni chanzo cha fursa nyingi za ajira serikalini na sekta binafsi na hata kujiajiri mtu binafsi.

Anataja baadhi ya njia zinazotumiwa na vijana kujiajiri ni pamoja na kutumia mitandao maarufu ya 'Upwork' na 'Fiverr', ambayo imekuwa ni majukwaa muhimu kwa vijana kuonesha uwezo wao na kupata ajira zinazowapa uhuru

wa kiuchumi.

Anabainisha kuwa, kwa sasa vijana wengi wanaweza kujiendeleza na kujiongezea ujuzi katika TEHAMA, kutokana na uwepo wa majukwaa mengi kama vile 'Coursera' na 'Udemy', ambayo yanatoa njia ya kupata elimu bora kwa gharama nafuu, na kuhimiza vijana wengi kutumia fursa hiyo kujiendeleza katika teknolojia ili kukuza utaalamu wao.

Frank anasema kuwa, TEHAMA ina nafasi kubwa katika kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika jamii zetu, ikiwemo kutumia Teknolojia ya 'Internet of Things' (IoT), inayotoa suluhu kwa masuala ya nishati mbadala, ambapo zinaweza kutengeneza bunifu zinazohusiana na uzalishaji wa nishati au vifaa vya ki-electroniki kwa matumizi ya ndani.

"Bunifu hizi pia zitakuwa ni suluhisho la kupunguza utegemezi kwa nchi za nje na kuongeza uwezo wetu katika sekta za viwanda na uzalishaji," anasisitiza Bw. Frank.

Aidha, anabainisha kwamba mifumo ya teknolojia kama Akili Mnemba (AI) na Machine Learning (ML), zimekuwa na mchango mkubwa katika kubuni suluhu katika sekta za afya na kilimo.

Bw. Alex anasema, katika miaka ya hivi karibuni TEHAMA imetoa fursa kwa vijana wa Tanzania kujiingizia kipato kwa kufanya biashara kupitia mitandao ya kijamii kama Instagram, WhatsApp, na tovuti zao binafsi, na hivyo kuongeza kipato chao na kusaidia uchumi wa nchi.

**"Uwepo wa majukwaa kama 'YouTube', 'podcaster' na utengenezaji wa aplikesheni tumizi, umeongeza wigo wa fursa kwa vijana kuonyesha ubunifu wao na kujiajiri kupitia njia za kidijitali, hii ni faida kubwa kwa taifa, kwani inasaidia kupunguza tatizo la ajira na kuongeza kiwango cha ushiriki wa vijana katika kujenga uchumi wa nchi kidijitali."**

Bw. Frank Alex
**Afisa TEHAMA**

Aidha, Bw. Alex ameishauri Serikali kuendelea kuwekeza katika elimu ya TEHAMA kuanzia ngazi ya msingi, sekondari hadi Vyuo Vikuu, ili kuhakikisha vijana wengi wanapata ujuzi wa kimsingi wa fani hiyo wakiwa katika umri mdogo.

Anasisitiza kuwa, ni vema Serikali ikaanzisha na kuendeleza vituo vya tafiti na ubunifu *(Research and Innovation Centers*) katika vyuo vikuu na shule za sekondari, ili kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha ubunifu wa vijana na kuwawezesha kutafuta suluhisho la matatizo ya kijamii kupitia TEHAMA.

Frank anaamini kuwa, uwepo wa vituo hivyo utasaidia vijana wengi kukuza vipaji vyao katika TEHAMA, kwa kutengeneza mifumo na bunifu zinazoweza kutatua changamoto mbalimbali za kiuchumi, afya, kilimo na kijamii.




Bw. Frank Alex kutoka katika kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao akielezea kuhusu bunifu mbalimbali zinazofanywa na kituo hicho wakati wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kilichofanyika Februari 11 - 13 Mwaka huu jijini Arusha

# WATUMISHI WAASWA KULINDA AFYA ZAO



Dkt. Hafidh Ameir, Afisa anayeratibu Afua za VVU mahali pa kazi ngazi ya taifa, katika sekta ya umma kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

*Na Catherine Peter*

Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wametakiwa kulinda na kuimarisha afya zao kwa kufanya mazoezi mara kwa mara, ili kuepukana na hatari ya kupata magonjwa sugu yasiyoambukizwa.

Hayo yalisemwa na Dkt. Hafidh Ameir, Afisa anayeratibu Afua za VVU mahali pa kazi ngazi ya taifa, katika sekta ya umma kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Februari 27 mwaka huu, wakati wa kikao cha mwaka cha watumishi jijini Dar Es Salaam.

Alibainisha kuwa, asilimia kubwa ya watumishi wa umma wapo katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo ugonjwa wa shinikizo la damu na kisukari, hali inayosababishwa na kutokuwa na utaratibu wa kufanya mazoezi mara kwa mara pamoja na ulaji wa vyakula usiozingatia lishe bora.

“Ili tuweze kujilinda dhidi ya magonjwa haya, ni lazima tujenge utaratibu wa kufanya mazoezi mepesi ya kutembea kwa dakika chache kila baada ya saa moja tunapokuwa kazini, ili kuruhusu damu kuzunguka mwilini, kwani tunatumia muda mwingi kukaa bila kuinuka,” alisema Dkt. Ameir.

Aliongeza kuwa, ni vizuri kuzingatia mlo kamili na kujiepusha na vyakula vya viwandani ambavyo huchangia kwa kasi uwezekano wa kupata magonjwa sugu yasiyoambukiza.

Naye Daktari wa Magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road Dkt. Maguha Stephano, aliwahimiza watumishi kujenga utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kubaini dalili za awali za ugonjwa wa saratani.

Alisema kuwa, utaratibu wa kupima afya mara kwa mara ni muhimu kwani huwezesha kubaini hatua za awali za ugonjwa wa saratani na hivyo kuweza kutibika mapema, na ikiwa dalili zitaonekana katika hatua za mwisho huwa na uwezekano mdogo wa kupona kwa mgonjwa.

**“Changamoto tuliyonayo ni wagonjwa kuja hospitalini kwa kuchelewa wakiwa wameshazidiwa unakuta ule ugonjwa tayari umeshakomaa na hautibiki tena, lakini kama mgonjwa huyu angewahi mapema ageweza kupona.”**

Dkt. Maguha Stephano
**Daktari wa Magonjwa ya Saratani**

Aliongeza kuwa, utaratibu wa kupima afya mara kwa mara si kwa ajili ya kuangalia VVU peke yake bali hata kwa magonjwa yasiyoambukiza kama vile saratani, na wakati mwingine inaweza kuwa ya kurithi hivyo tahadhari zikachukuliwa mapema.

Aidha, Mtaalamu wa afya ya akili kutoka Taasisi ya Afyachek Dkt. Isaac Maro, aliwataka watumishi wa Mamlaka kutunza afya ya akili ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza baadaye.

Alisema, afya ya akili ni muhimu kwa ustawi wa mwanadamu, hivyo ni lazima watu wote wajifunze kuweka usawa wa maisha kwa kutenga muda wa kazi, muda binafsi na muda unaohitaji kushiriki mambo mbalimbali ya kijamii.

“Watu wengi wanapata changamoto ya afya ya akili kwa kuwa na msongo mkubwa wa mawazo na kushindwa kuweka usawa katika maisha ya kila siku, muda wa kazi utumike kazini na muda binafsi utumike kwa mambo binafsi”, alisema Dkt. Maro.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa watu kuzungumza na watu wakaribu yao au wataalam wa saikolojia wanapopata changamoto za kimaisha ili kupata ushauri sahihi na kwa wakati na kuepukana na kufanya maamuzi yasiyo sahihi ikiwemo kujiingiza katika ulevi wa kupindukia au kujiua.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## MAONESHO :
## KIKAO KAZI CHA 5 CHA SERIKALI MTANDAO




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Utafiti, Mafunzo na Ubunifu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Dkt. Jaha Mvulla, wakati alipotembelea banda la Maonesho la e-GA wakati wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao.




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) Bw. Dennis K. Simba, alipotembelea banda la Maonesho la PPRA wakati wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao.

# KIKAO KAZI CHA 5 CHA SERIKALI MTANDAO



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba akitoa wasilisho kuhusu ukuaji wa Serikali Mtandao nchini wakati wa Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kilichofanyika kuazia tarehe 11-13 Februari Jijini Arusha.




Washiriki wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao wakisikiliza mada mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa kikao kazi hicho.

# SHUKRANI



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango (kulia), akipokea tuzo maalum ya kuthamini mchango wake katika kukuza matumizi ya TEHAMA Serikalini kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Goerge Simbachawene (Mb).



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, akimkabidhi tuzo ya shukrani kwa kudhamini kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Mifumo na Huduma za TEHAMA - Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Angelina Miso

# KIKAO CHA WATUMISHI WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



Kaimu Meneja wa Vihatarishi na Ubora wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Bi. Farida Juma, akitoa elimu kuhusu kiwango cha kimataifa kinachotoa miongozo ya Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Taarifa..



Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa kikao cha watumishi, kilichofanyika Februari 26-28 katika Ukumbi wa Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam.

# BARAZA LA WAFANYAKAZI



Viongozi wa baraza la wafanyakazi la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wakisiliza hoja mbalimbali kutoka kwa watumishi, wakati wa kikao cha baraza kilichofanyika Januari 28 mwaka huu katika Ukumbi wa Midland Inn jijini Dodoma



Wajumbe wa baraza la wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakiwa katika kikao cha baraza hilo kilichofanyika Januari 28 mwaka huu katika Ukumbi wa Midland Inn jijini Dodoma

# BONANZA LA WATUMISHI




Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakishiriki mchezo wa kuvuta kamba, wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu, katika viwanja vya Gymkhana.




Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakishiriki mchezo wa mpira wa Miguu, wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu, katika viwanja vya Gymkhana.

# BONANZA LA WATUMISHI



Watumishi wanawake wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakishiriki mchezo wa mbio fupi, wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu, katika viwanja vya Gymkhana.



Watumishi wanaume wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wakishiriki mchezo wa kukimbiza kuku, wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu, katika viwanja vya Gymkhana.

# WASHINDI



Wachezaji wa timu ya Mpira wa Miguu ya Dodoma wakishangilia ushindi walipokabidhiwa kombe mara baada ya kuifunga timu ya Dar Es Salaam kwa magoli 2-0 , wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu katika viwanja vya Gymkhana.



Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji CPA. Salum Mussa, akimkabidhi zawadi Afisa TEHAMA Bw. Salum Mohamed mara baada ya kuibuka mshindi katika mbio za mita 100 wakati wa bonanza la michezo kwa watumishi lililofanyika Februari 28 mwaka huu, katika viwanja vya Gymkhana.

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI
Mhandisi Benedict B. Ndomba

Mkurugenzi Mkuu

## WAJUMBE
CPA (T) Salum Mussa

Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji

SACP Hamis Ali

Mkaguzi Mkuu wa Ndani

SACP Rafael Rutaihwa

Meneja wa Huduma za Sheria

Long'ida Oltetiai

Meneja wa Huduma kwa Wateja na Tawimu

## MHARIRI
Subira Kaswaga

Meneja Mawasiliano


## WAANDISHI
Catherine Peter | Afisa Habari Mwandamizi

Queenter Mawinda | Afisa Habari Mwandamizi

## WAPIGA PICHA
Mussa Enock |Afisa Habari

Ben Bago |Afisa Habari

## MSANIFU KURASA
Edger Msamba | Afisa TEHAMA




## Furahia Huduma za Serikali kiganjani mwako kwa kubofya

***152*00#**